



## BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

### ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

#### BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

#### MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 18 Mei, 2022**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi  
na Dua zitasomwa.

#### I. HATI ZA KWASILISHA MEZANI:

##### Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka 2022/2023.

##### Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa Mwaka 2022/2023.

#### II. MASWALI:

##### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

156. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Zanzibar ina uwakilishi wa balozi ndogo ndogo mbali mbali zinazoiwakilisha nchi kimataifa.

- (a) Ni balozi ngapi ndogo ndogo zenyé uwakilishi wake

Zanzibar.

- (b) Ni fursa zipi za kielimu, kiuchumi na ajira ambazo wananchi wetu wananaufaika nazo kupitia balozi hizo.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi wa Uwekezaji:**

183. MHESHIMIWA SHADYA MOHAMED SULEIMAN (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Serikali imewapatia wananchi wake hasa kina mama mikopo yenye masharti nafuu.

- (a) Je, kina mama ambao tayari wameshakamilisha masharti yote ni lini watapatiwa fedha hizo.
- (b) Je, ni vikundi vingapi vya kina mama wa Mkoa wa Kusini Pemba vyenye sifa ya kupata mikopo hiyo.
- (c) Je, ni kiasi gani cha fedha kilichotengwa kwa kina mama hao ambao watakuwa na sifa ya kupewa mikopo hiyo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

32. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Utumishi wa Umma, ilitoa barua ya maelekezo kuhusu posho inayotolewa kwa ajili ya ufiwa kwa Watumishi wa Umma.

- (a) Je, kwa nini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inalipa chini ya kiwango kilichoelekezwa.
- (b) Ni sababu gani zinazopelekea fedha hizo kuchelewa kutolewa kwa wafanyakazi wa Wizara hii pale wanapowasilisha maombi yao.
- (c) Je, Wizara imefanya jitihada yoyote kuwapatia elimu watumishi wake juu ya stahiki hiyo ili wakifiwa waiombe.

137. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na malalamiko kwamba Serikali, kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imekuwa ikidharau na kupuuza ushauri na maelekezo ya Bodi ya Madaktari na kufanya maamuzi bila ya kuzingatia ushauri wa Bodi ya Madaktari, yakiwemo mambo yanayowahusu Watu Wenye Ulemavu.

- (a) Je, Serikali, kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ina msimamo gani kuhusu maamuzi ya kitaalamu yanayotolewa na Bodi ya Madaktari ya Zanzibar.
- (b) Je, kwa nini Serikali, kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imekuwa ikitilia mashaka maamuzi ya kitaalamu ya Bodi ya Madaktari ya Zanzibar.
- (c) Je, ni kwa sababu zipi Serikali, kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, huwapeleka watumishi kutaka ushauri wa Bodi ya Madaktari ya Zanzibar.

#### **Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

120. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)  
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ni jambo la kufurahisha kwamba, takriban Serikali zote zilizopita zimeahidi kuitengeneza barabara ya Maziwani-Mtijuu iliyomo ndani ya jimbo la Pandani. Hata hivyo, inasikitisha kwamba barabara hiyo imepuuzwa katika awamu zote kinyume na ahadi tajwa. Kwa sasa, barabara imekuwa ikihatarisha maisha ya watu hasa wagonjwa na mama wajawazito.

- (a) Je, ahadi za kuitengeneza barabara hiyo bado zipo na kwa nini Serikali imeshindwa kuzitekeleza.
- (b) Kwa kuwa wananchi wa Maziwani na vijihi jirani waliwahi kuchangishwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo, Je, ni kiasi gani cha michango hiyo kilipatikana kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo.
- (c) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kuitengeneza barabara hiyo pamoja na daraja la Kwa Foum-Mtambwe (Bahanasa – Pembeni).

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

95. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) -  
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa na jitihada mbali  
mbali za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

Je, suala hilo limefikia hatua gani.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika  
Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale  
kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,  
18 Mei, 2022.



(Raya Issa Msellel)  
**KATIBU WA BARAZA**